Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 78 No. 196 | SHAWW-DH. QAD 1439 AH | AGOSTI 2018 | ZAHOOR 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na Hatukumtuma kabla yako Mtume ye yote ila Tulimfunulia ya kwamba hakuna aabudiwaye ila Mimi, basi Niabuduni..... (21:26)

Watu Walio Bora Kabisa



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 06/07/2018, baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema: Katika siku za hivi karibuni, nimekuwa nikitoa tawasifu ya baadhi ya Masahaba (ra) wa Mtume Mtukufu (saw), ambao walishiriki katika Vita ya Badr. Wengi miongoni mwa Masahaba(ra) nitawataja leo tawasifu zao nitazitoa tu kwa kifupi sana. Hadhrat Subaib bin Qais bin Esha (ra). Alishiriki katika Vita ya Badr na Uhud. Jina la mama yake alikuwa ni Khadija binti Umar bin Zaid. Alikuwa na mtoto wa kiume aliyeitwa Abdullah ambaye alifariki utotoni, ambaye mama yake alikuwa ni wa kabila la Banu Jazara. Alikuwa hana watoto wengine. Hadhrat Unais bin Qitada (ra) ambaye alifariki katika Vita ya Uhud. Yeye pia alikuwa hana mtoto yeyote. Kutokana na Hadithi moja, Hadhrat Khansa binti Khuddam (ra) aliolewa na yeye wakati alipopata Ushahidi. Hadhrat Malail bin Wabra (ra). Alishiriki katika Vita ya Badr na Uhud, zote mbili. Alikuwa na watoto wawili, Zaid na Habiba (ra) ambao mama yao alikuwa ni Umm Zaid bint Nazla bin Malik (ra). Uzao wake haukuendelea baada ya watoto wake. Kutokana na Hadithi moja, aliambatana na Mtume Mtukufu katika Vita ya Badr, Uhud na vita zote zingine. Hadhrat Naufil bin Abdullah bin Nazla. Alipata Ushahid katika vita vya Uhud. Alishiriki katika Vita vya Badr na Uhud. Ukoo wake haukuendelea pia.

Hadhrat Wadee'a bin Amar (ra). Alikuwa ni wa kabila la Banu Juhaina ambalo lilikuwa na unasaba na Banu Najar. Alishiriki katika Vita ya Badr na Uhud.

Hadhrat Yazeed bin Munzir bin Sar bin Khunas (ra). Alikuwa ni wa kabila la Banu Khazraj na alishiriki katika Baiati iliyofanyika 'Uqba. Mtume Mtukufu (saw) aliweka muungano wa kindugu kati ya Hadhrat Yazeed bin Munzir (ra) na 'Amir bin Rabi'ah (ra). Alishiriki katika Vita za Badr na Uhud. Alikuwa hana watoto wakati anafariki.

Endelea uk 4

Katika Ufunguzi wa Msikiti Mongella atangaza Vita Dhidi Ya UKIMWI Na Dawa Za Kulevya

Na Pazi Mazongera
Shinyanga

Nawapongeza taasisi ya Ahmadiyya kwa kutoa huduma za kijamii na nawapongeza viongozi wenu ambao wanashirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya, kwani vita hii ni ya kwetu sote. Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mh. John Mongella katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naib Meya wa Jiji la Mwanza, Mheshimiwa Bhiku Kotecha ambaye ni diwani wa kata ya Nyamagana katika hafla ya ufunguzi wa Msikiti mkubwa wa Ahmadiyya jijini Mwanza.

Masjid Baitul Kabiir uliopo Nyegezi jijini Mwanza



Amir sahib Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akikata utepe katika ufunguzi wa msikiti mpya wa jijini Mwanza

Mkuu wa Mkoa alisema, viongozi wa dini wana wajibu wa kuhakikisha sehemu za ibada zinatumika kwa ibada tu bila ya mambo mengine na watu kuheshimiana kwa dini zao bila ya ubaguzi, alisisitiza Mkuu wa Mkoa.

Amani tuliyonayo ni tunu kubwa tuliyobarikiwa katika nchi yetu hivyo ni lazima kuiendeleza na kujivunia kwani wako waliokosa na wana mashaka makubwa, alisema.

Katika hafla hiyo ya kihistoria katika jiji la Mwanza, Mkuu wa Mkoa aliishukuru Jumuiya ya Ahmadiyya kwa kumualika kuwa mgeni rasmi kwenye ufunguzi wa msikiti mkubwa uliopo hapa Nyegezi Calfornia jijini Mwanza na kuwapongeza wale wote waliofanikisha ujenzi wa msikiti huo.

Watu wapatao zaidi ya mia sita walihudhuria ufunguaji wa msikiti huo wakiwemo pia Makamanda wa vikosi vya ulinzi na usalama, Waheshimiwa madiwani watano wa Mkoa wa Mwanza.

Katika ufunguzi huo uliohudhuriwa pia na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundry na viongozi mbalimbali wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika Mkoa wa Mwanza akiwemo Rais wa Jamaat ya Kanda ya Ziwa Mzee Salum Abdallah Thanni na Mbashiri wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa Sheikh Waseem Ahmad Khan utabakia kwenye kumbukumbu za watu kwa muda mrefu kuleta hamasa na furaha kubwa kwa wakazi wa jiji la Mwanza.

Baada ya ufunguzi huo kufanyika yalifanyika maombi ya kimya yalioongozwa na Amir Sahib na baadaye kupiga picha ya pamoja na viongozi na watu mbalimbali waliohudhuria.



Waumini na wageni mbalimbali waliofika katika ufunguzi wa msikiti

Ukhalifa ndio Taa ya Islam - Jibu kwa Al Huda Uk.8

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SHABAHA YA KUUMBWA KWETU

Wanafalsafa wanaotajwa kwa umahiri na uwezo wao wa kuchambua mambo, kukifikia kiini na kwa jicho kali kutizama mbegu ya wakati na kumaizi ipi itakayoota na itakayokuwa si riziki, wamekuwa wakisumbuliwa na kujishughulisha na masuala yafuatayo:-

- Maisha ni nini?
- Kwa nini tupo hapa?
- Shabaha ya kuumbwa kwetu ni nini?

Miongoni mwa wanafalsafa hao ni; Plato na Aristotle wa Uyunani, Spinoza wa Spain, Betrand Rusell wa Uingereza, Hobbes wa Uingereza na John Stuart Mill wa Uingereza kwa kuwataja wachache.

Na waandishi mahiri wa Fasihi wenye vilemba viwili kimoja cha fasihi na kingine cha Falsafa hao ni pamoja na William Shakespear wa Uingereza, Goethe wa Ujerumani, Walt Whitman wa Marekani, Victor Hugo wa Ufaransa, Leo Tolstoy wa Urusi, Emily Bronté wa Uingereza na Dostovesky wa Urusi kwa kuwataja wachache.

Wote kwa ujumla wao wamejenga nyumba yao kwenye mchanga na ndio maana tunaiona sio imara. Kwa mathalan E.M. Foster katika riwaya yake *A Passage to India* anasema maisha ni upuuzi mtupu na hakuna chochote na wale wote wanaosema ya kwamba kuna shabaha na sababu ya kuwepo kwetu hapa wanataka kuhalalisha tu kuwepo kwao lakini maisha ni upuuzi na yanachosha. Karl Marx anasema ya kwamba binadamu si chochote isipokuwa maada ambayo inaathiriwa na hali ya siasa na uchumi na baadaye inarudi kwenye mchanga na hiyo ndiyo mwisho wa habari yake.

Ndiyo maana tunasema, nyumba waliyoijenga ni dhaifu mithili ya nyumba ya Ankabut kwani wameweka mkokoteni mbele na farasi nyuma bila shaka safari hiyo haiwezi kufanyika. Jambo ambalo walitakiwa kuanza nalo ni kutafuta kwa udi na uvumba aliyeumba dunia hii. Ni dhahiri binadamu hakushiriki katika kupanga kuja hapa duniani. Hapakuwepo bunge wala upigaji wa kura kwamba mimi nina hamu na shauku ya kuja duniani. Ni wazi basi kwamba hakuna binadamu aliyeshiriki katika uamuzi wa kuja duniani na wala hatuna uamuzi wa lini tutoka duniani.

Kama tumekuja duniani pasi ya mapenzi yetu, uamuzi wetu, kushiriki kwetu, tunawezaje kufahamu shabaha yetu ya kuja duniani? Kila ukikiona pale usidhani kimeota kama uyoga (na uyoga umeoteshwa na muoteshaji). La hasha! Kimetengenezwa na seramala; ndiye anayefahamu vizuri shabaha ya kukitengeneza kiti. Anaweza kukiuza au kukikalia yeye mwenyewe. La msingi hapa ni kwamba ni seremala anayejua shabaha ya kutengenezwa kwa kiti.

Wanafalsafa hawa na waandishi hawa mahiri wangebahatika kusoma Qur'an Tukufu wasingepata taabu ya kutegua kitendawili hiki. Hapana shaka baadhi wamesoma Qur'an Tukufu. Lakini masikini ni kule kupitia na kukigusa bila ya kufahamu maana za ndani za Qur'an Tukufu na ndiyo maana Allah Anasema "*Hawaigusi ila waliotakasika*". Kazi hiyo ya kufafanua maana za ndani za Qur'an Tukufu amepewa mwana wa kiroho wa Mtukufu Mtume s.a.w. Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Ni sultani huyo wa kalamu kwa kupitia wahyi ambaye ameweka bayana lulu zilizokuwa zimefichwa kwa wale wasiokuwa na jicho la yakini. Uwezo huu na msaada huu mkubwa amepewa Masihi Aliyeahidiwa na Allah kutokana na mapenzi yake makubwa kwa Mbora wa viumbe, sababu ya kuumbwa kwa dunia, Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w.

Ni elimu ya ajabu juu ya Qur'an Tukufu aliyopewa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Ndiye aliyefafanua vizuri mafundisho yaliyomo katika Qur'an Tukufu. Amesisitiza hakuna hata nukta moja iliyofutika na kuachwa na Qur'an Tukufu. Ina ulinzi uliokamilika. Mpangilio wake ni wa hekima tupu. Na sheria iliyokamilika na ya mwisho kuja kwa binadamu.

Kwa kutumia Qur'an Tukufu Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametoa ushahidi wa kuumbwa kwa binadamu. Allah Amemuumba binadamu ili amtambue, amuabudu na kumpenda.

Swala la msingi la kujiuliza je binadamu anawezaje kuipata shabaha hiyo tukufu ya kuumbwa kwake? Masihi Aliyeahidiwa amefafanua njia nane:

1. Kumtambua Mungu wa kweli.
2. Kufahamu uzuri na sifa za Allah. Uzuri ni furaha ya dawamu na uzuri siku zote unavuta moyo.
3. Kufahamu kadiri unavyoweza neema za Allah. Ni jitihada tu kwani huwezi kuzihesabu neema za Allah.
4. Sala.
5. Kujitolea mali na uwezo wako wote kwa ajili ya Allah.
6. Subira.
7. Kukaa na watu wema.
8. Njozi za kweli, wahyi kutoka kwa Allah.



JUMANNE RAJABU,
AHMADIYYA JAMAL,
S.L.P 1,
MOROGORO,

1/7/2018

MHARIRI,
ALHUDA,
S.L.P 90399,
DAR ES SALAAM.

MAKALA: UONGOZI WA UKHALIFA NDIO UNGOZI PEKEE WA KIROHO NA SAHIHI KUFUATWA KATIKA DINI YA ISLAMU.

Asalaam Alaikum Warahmatullah Wabarakatuhu Ama baad. Pamoja na barua hii naambatanisha makala yenye kichwa cha habari kama ilivyoonyeshwa hapo juu kwa madhumuni ya kuchapishwa katika gazeti lako la ALHUDA kwa kusomwa na ndugu zetu Waislamu na wasio waislamu.

Ni matumini yangu utakuwa muadilifu kwa hili.

Ndimi wako,

.....

JUMANNE RAJABU

Nakala: Mhariri Mapenzi ya Mungu
S.L.P 376 DAR ES SALAAM

AL – HUDA, Swawal 1439 H. ALKHAMIS JUNI 2 8 – JULAI 4. 2018

: UKADIANI SI DHEHEBU WALA SII KUNDI LA KIISLAMU.

Bwana Jumanne Rajabu wa Morogoro amedhihirisha mapenzi yake makubwa kwa Jamaat Ahmadiyya. Kalamu yake haionyeshi kuishiwa wino kila anapoona Jamaat Ahmadiyya inasakamwa. Pamoja na umri mkubwa alionao, yeye hushika kalamu na kuingia kwenye kitali na sote tunafahamu hakuna silaha bora katika Jamaat Ahmadiyya kuliko kalamu. Lakini kalamu haiwezi kufanya kazi vizuri iwapo hatujijengei utamaduni wa kusoma.

kwa msaada wa Allah tunavyo vitabu vingi katika lugha yetu ya Kiswahili. Sifa moja kubwa ya Mzee Jumanne Rajabu ni mapenzi yake makubwa ya kupenda kusoma. Huu ni utamaduni ambao tunatakiwa tuendelee kuujenga bila kujali iwapo mtu ni kijana au mzee. na kila apataye chochote asifanye ubakhili bali awagawie wenzie kama anavyofanya bwana Jumanne Rajabu.

Makala yake kwenye ukurasa wa 8 ni ushahidi tosha wa mwanajamaat ambaye anatafuta kila tunapoonewa kwa masingizio yasiyo kichwa wala miguu na hapo kuchukua hatua ya kuweka taswira safi ya mafundisho ya Islam. Na kwa hakika mafundisho ya Islam kwa hivi sasa hayapatikani katu nje ya Ahmadiyya na hazina kubwa inapatikana katika vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Kuvisoma vitabu hivyo ni wajibu kwa kila Muislam.

Ni matumaini yetu Mhariri wa gazeti la Al Huda atakuwa muadilifu kwa kuichapisha makala ya majibu ya shutuma dhidi ya Jumuiya ya Ahmadiyya. Na kwa sababu Waislamu ni waadilifu katu hatuna shaka na hilo.

Shumbe mwana wa Rajabu
Lakosha lako jawabu
Akubariki Wahabu
Dini kuitumikia

Na Mhariri wa Huda
Rajabu kaleta mada
Nadhani hakuna shida
Gazetini kuitoa

Mhariri

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Islam na Malezi Bora ya Watoto

Mwl **Issa Salum Disowile**
Shule ya Sekondari Ahmadiyya

Kutoka toleo Lililopita



Mwl **Issa Salum Disowile**
Mwandishi wa Makala hii

MAWASILIANO NA MTOTO AKIWA TUMBONI NA BAADA YA KUZALIWA.

Sayansi inathibitisha kwamba "watoto wanaweza kusikia wakiwa tumboni, pia baada ya kuzaliwa wanaweza kuitikia (react) au kuzihisi sauti zilizorekodiwa ambazo wamekuwa wakiziishi baada yake." (Penelope Leach, *The Essential First year* (DK, 2010), 75)

Na huu ndio ukweli ambao unalezea kwanini uislam unasisitiza kwamba mama mjamzito asome sana Qur'an katika kipindi chake chote cha ujauzito. Wanamama wengi wa kiislamu wanashuhudia kwamba baada ya kusoma Qur'an wakiwa wajawazito, watoto wao huwa wanafurahi au wanajitingisha pindi wanapowasomea tena baada ya kuzaliwa.

Mtume Mtukufu Muhammad(s.a.w) alisema kwamba mtoto azaliwapo, adhaana isomwe kwenye sikio lake la kulia na iqaama katika sikio lake la kushoto.

Hadhrat Mirza Bashir-ud-din Mahmud Ahmad(r.a) Khalifa wa pili akielezea juu ya hili alisema: "***Uislamu umeelezea ukweli huu mkubwa na kusema kwamba mafunzo kwa mtoto sio tu yaanze wakati wa kuzaliwa, bali yaanze kabla ya kuzaliwa. Mimi nafikiri kwamba Mtume Mtukufu(s.a.w) angeenda nyuma zaidi. Angeweza kueleza kwamba mafunzo ya mtoto lazima yaanze wakati mtoto bado akiwa tumboni mwa mama yake. Kwahiyo Mtume Mtukufu(s.a.w) anaeleza kwamba mafunzo kwa mtoto yaanze wakati wa kuzaliwa.***

Jambo la kwanza ni kusoma adhaana (wito wa waislam kwenye sala) katika sikio la mtoto wakati wa kuzaliwa. Hakuna mtu anaweza kufikiri kwamba hii ni sehemu kubwa ya muujiza. Maneno yote ya adhaana na iqaama hunasa katika akili ya mtoto. Aidha ni ukumbusho kwa wazazi kwamba wanawajibu kwa maisha ya mtoto huyu. Mafunzo ya maisha hayo sasa ni wajibu wao. Inayoanza tangu kuzaliwa kwake. Mbali na Adhaana, Mtume Mtukufu(s.a.w) ameweka wazi kuwa watoto wanapaswa kufundishwa tabia njema tangu utoto wao." (ways of the seekers: p.48)

KUNYONYESHA WATOTO

Qur'an Tukufu inatoa mwongozo juu ya kunyonyesha na kumtunza mtoto kuanzia anapozaliwa na pia inasisitiza wajibu wa baba katika malezi.

"***Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha; na ni juu ya baba yake chakula chao na nguo zao kwa sheria; wala nafsi yo yote isikalifishwe ila kwa kadiri ya wasaa wake***." (Al-Baqara: 234)

Hii inamaana kwamba kunyonyesha mtoto ni mpaka miaka miwili, lakini inaruhusiwa kusitisha kunyonyesha kabla ya miaka miwili kuisha, endapo baba na mama wote kwa pamoja watakubaliana jambo hili. Aya hii pia inaashiria kwamba mtoto asiachishwe kunyonya kabla miaka miwili haijaisha bila ya ridhaa ya mama.

Wanasayansi hivi karibuni wameeleza faida za kunyonyesha mtoto maziwa ya mama, ambapo faida hizi zinaanza siku ya kwanza na zinaendelea kwa miaka mingi. Maziwa ya mama yana virutubisho ambavyo humsaidia mtoto kukua vizuri, pia maziwa ya mama yana chembe chembe ambazo humsaidia kumlinda mtoto dhidi ya magonjwa, na faida zingine nyingi.

Baada ya kunyonya maziwa, ambapo kwa kawaida tunashauriwa ndani ya miezi sita ya mwanzo ya kuzaliwa mtoto, maziwa ndiyo chakula pekee cha mtoto, wala mtoto asipewe kitu kingine chochote zaidi ya hayo maziwa kwa kipindi hiki cha miezi sita, kwa sababu mfumo wake wa mmeng'enyo unakuwa haujakomaa sawa sawa, hivyo maziwa pekee yanafaa. Na ifahamike tu kwamba maziwa ya mama huendelea kubadilika ili kukidhi haja ya mtoto kwa kadri mtoto anavyoendelea kukua.

Baada ya miezi sita wazazi wanaanza kumtengenezea chakula kama vile uji wa lishe ili mtoto wao aendelee kukua vizuri. Ukuaji na tabia ya mtoto huathiriwa na chakula. Chakula kizuri chenye virutubisho vyote kitamsaidia mtoto kuwa na afya njema na kukua vizuri. Baadhi ya watoto hukosa vyakula vyenye virutubisho , hali hii huathiri umakini na tabia ya mtoto kwa ujumla.

Juu ya chakula Qur'an Tukufu inatuongoza na kutufundisha kama ifuatavyo "***Enyi mlioamini, kuleni katika vitu vizuri Tulivyowaruzukuni, na Mshukuruni Allah, ikiwa mnamwabudu yeye tu***." (Al-Baqara: 173)

NJIA SAHIHI ZA MALEZI KWA WATOTO

Tunapaswa kutengeneza picha kubwa ya baadae, kwa kutafakari juu ya athari za muda mrefu za baadae zinazotokana na matendo ya muda mfupi. Uchaguzi mzuri wa kuishi wa sasa unaathiri baadae ya watoto wetu. Yaani tunavyojichagulia namna ya kuishi leo ndivyo watakavyoishi watoto wetu kesho.

Tunapaswa kutambua kwamba matendo yetu yanaongea zaidi kuliko maneno yetu. Hivyo twatakiwa kuwa mfano kwa watoto wetu katika kila kitu chema na kutambua kwamba kulea mtoto siyo kazi au mzigo, bali ni sehemu ya maisha. Na maisha yenye afya na ya maana tu ndiyo tunayotakiwa kuyaishi.

Tukumbuke ya kwamba tabia nyingi ni rahisi kuigwa na kurithiwa na watoto katika miaka ya mwanzo ya malezi, vilevile tabia mbaya zinazorithiwa na watoto katika miaka hii ya mwanzo ni ngumu sana kuziondoa au kuzirekebisha ukubwani.

Tukumbuke ya kwamba tabia nyingi ni rahisi kuigwa na kurithiwa na watoto katika miaka ya mwanzo ya malezi, vilevile tabia mbaya zinazorithiwa na watoto katika miaka hii ya mwanzo ni ngumu sana kuziondoa au kuzirekebisha ukubwani. ***Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo***. Hivyo twapaswa kupandikiza tabia njema kwa watoto wetu tangu mwanzo, inamaanisha wazazi wanatakiwa kuishi kwa mujibu wa mafundisho ya Islam mapema.

Tunapaswa kutambua kwamba katika miaka hii ya mwanzo mtoto anajifunza kwa kuiga au kufuata maelekezo, hata hivyo wakiwa wakubwa, tunapaswa kuwafundisha na kuwaongoza katika kutengeneza chaguo zao wao wenyewe. Kama inavyosemwa, "mpe mtoto samaki atakula kwa siku moja na kumaliza, lakini mfundishe mtoto kuvua samaki, atakula maisha yake yote." Mtoto anatakiwa kujifunza kutofautisha zuri na baya na matokeo yake, ili aweze kufanya maamuzi juu ya chaguo lake wenyewe.

Tunapaswa kuwa thabiti na imara katika malezi yetu. Ni muhimu kwa wazazi wote kuwa kitu kimoja na kufanya kazi pamoja wakisaidiana kutika kutimiza lengo hili la malezi bora kwa watoto. Wazazi wanapogombana au kutofautiana wanaharibu na kuathiri watoto kisaikolojia, kiakili na kihisia pia.

Ni muhimu kwa wazazi wapya na vijana kubadilika kitabia, waache tabia za ujana na kuiishi Islam katika majumba yao, wapende ndugu zao, wajiheshimu, wafanye mambo yao kwa hekima, pia wawe na huruma kwa kila mtu, ili watoto waige au wapate mafundisho sahihi ya Islamu juu ya namna ya kuishi.

BAADHI YA KANUNI ZA KIISLAMU KATIKA MALEZI

Tuangalie baadhi ya kanuni za Islamu juu ya kulea watoto. Jamii zetu zinahubiri uhuru wa kujiamulia mambo ya kufanya. Lakini dini tukufu ya Islamu inatuonyesha zuri na baya, na kutuongoza katika chaguzi sahihi:

DUA

Jambo la kwanza kabisa, katika malezi yetu lazima tuanze na kuomba dua kwa Allah, kama ambavyo nimekwisha tangulia kusema. Qur'an Tukufu inatufundisha kuomba kwa ajili ya kizazi chema kama tunavyosoma kwa Nabii Zakaria (a.s): "***Mola wangu, Unipe kutoka Kwako wazao wazuri; kwa yakini Wewe ndiwe Usikiaye maombi***." (Al-Imrani: 39)

Kwa hiyo wazo la kulea watoto wa Islam lazima liwepo akilini mwetu hata kabla watoto wetu huzaliwa. Siyo tu tuwaombee watoto pekee yao bali pia wake zetu na sisi wenyewe. Kama nilivyokwisha kueleza mwanzo kwamba tuombe: "***Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na Utujaalie kuwa viongozi***

Inaendelea uk. 5

Watu Walio Bora Kabisa

Kutoka uk. 1

Kaka yake, Maqir bin Munzir (ra), pia alishiriki katika Baiati ya 'Uqba na pia alishiriki Vita za Badr na Uhud. Kisha, kuna Sahaba aliyeitwa Hadhrat Khawaria bin Humayyar Ashja'i. Alikuwa ni wa kabila la Ashaja', ambalo lilikuwa ni rafiki wa kabila la Banu Khazraj. Jina la kaka yake ni 'Abdullah bin Humayyar, ambaye alishiriki naye bega kwa bega katika Vita vya Badr.

Hadhrat Suraqa bin 'Amr (ra). Alikuwa ni Ansari (yaani mkazi wa madina). Jina lake ni Suraqa bin 'Amr bin 'Atiya bin Hansaa Ansari (ra). Alifariki mwezi wa Jamadi-ul-Awwal (mwezi wa tano kwa kalenda ya mwezi) katika mwaka wa nane wa Hijra (kuhamia Madina) wakati wa vita ya Mu'tah. Jina lake kamili lilikuwa Suraqa bin 'Amr bin 'Atiya bin Hansaa Ansari. Mtume Mtukufu alifanya Mkataba wa udugu kati ya Nahja Maula 'Amr na Suraqa bin 'Amr (ra). Alishiriki katika vita za Badr, Uhud, Khandaq na Khaybar. Zaidi ya hapo, alibarikiwa pia kuwa pamoja na Mtume Mtukufu (saw) katika tukio la Mkataba wa Hudaibiyya na pia 'Umrat-ul-Qadha (hija ya kwanza Makka). Hadhrat Suraqa bin 'Amr alikuwa miongoni mwa wale masahaba wenye bahati, (ra) ambao walibarikiwa fursa ya kushiriki katika Bai'at-e-Ridhwan. Alikuwa hana ukoo wowote na alipata Ushahhid katika mwaka wa nane wa Hijra wakati wa vita ya Mu'tah.

Hadhrat 'Abbad bin Qais (ra). Yeye pia alifariki katika mwaka wa nane wa Hijra (kuhamia madina) wakati wa vita vya Mu'tah. Hadhrat 'Abbad walienda pamoja na Mtume Mtukufu (saw) wakati wa vita vya Badr, Uhud, Khandaq na Khaybar. Pia alishiriki katika Mkataba wa hudaibiyya.

Hadhrat Ab-uz-Zayyah bin Thabit bin Nu'man (ra). Alishiriki katika Vita vya Badr, Uhud na Khandaq pia katika Mkataba wa Hudaibiyya. Alipata Ushahhid katika mwaka wa saba wa Hijra wakati wa Vita ya Khaibar. Inasimuliwa kwamba Mayahudi mmoja alimpiga na kukata kichwa chake, na matokeo yake akawa Shahhid.

Hadhrat Ansa (ra). Alifariki wakati wa Vita vya Badr. Hadhrat Ansa (ra) alikubali Islam katika hatua zake za mwanzo mwanzo na alihamia Madina wakati wa kuhama. Alikuwa ni mgeni wa Hadhrat Sa'ad bin Khaithma (ra). Kipindi chote cha uhai wake shughuli yake aliyoipenda ilikuwa ni kumhudumia Mtume Mtukufu (saw). Alikuwa ni mtiifu kiasi hiki kwamba inasimuliwa kumhusu yeye kwamba hata alipokuwa akikaa, alikuwa akifanya hivyo baada ya kuomba ruhusa kutoka kwa Mtume Mtukufu (saw). Alipigana bega kwa bega na Mtume Mtukufu (saw) katika Vita vya Badr. Hadhrat Abu Kabsha Sulaim (ra). Wadhifa wake ni Abu Kabsha. Alifariki wakati wa Ukhalifa wa Hadhrat 'Umar (ra). Alikuwa ni mtumwa wa Kiajemi aliyeachiwa huru na Mtume Mtukufu (saw). Ni Sahaba aliyeshiriki katika Vita vya Badr. Alikubali Islam katika hatua za mwanzo mwanzo na alihamia Madina baada ya kupata ruhusa ya kufanya hivyo. Alipigana bega kwa bega na Mtume Mtukufu (saw) katika kila vita, ikiwemo vita vya Badr. Hazrat Marsad bin Abi Marsad (ra). Alifariki katika mwezi wa Safar (mwezi wa pili wa kalenda ya kimwezi) katika mwaka wa tatu wa Hijra. Alikuwa ni Sahaba aliyeshiriki katika vita vya Badr. Alikubali Islam katika hatua zake za mwanzo mwanzo na alihamia Madina kabla ya Vita vya Badr kuanza. Mtume Mtukufu alifanya Mkataba wa undugu kati yake na Hadhrat Aus bin Samit (ra). Katika siku ya Vita vya Badr, alifika akiwa amepanda farasi ambaye jina lake lilikuwa Sabal. Ibn Ishaq ameandika kwamba Hazrat Marsad, (ra) alikuwa ni kiongozi wa kundi lile la wanajeshi, ambalo Mtume Mtukufu (saw) alilipeleka Raji. Tukio hili lilitokea katika mwezi wa Safar katika mwaka wa tatu wa Hijra. Kutokana na baadhi ya wasimulizi, Hadhrat 'Asim bin Thabit alikuwa kiongozi wa kundi hilo. Tukio la kuwa kwake Shahhid ni kama ifuatavyo:- Banu 'Azl na Qarah walijifanya wameikubali Islam na walimuomba Mtume Mtukufu (saw) awapelekee baadhi ya walimu ili wapate elimu ya dini.

Hapo, Mtume Mtukufu (saw) aliwapelekea kundi la watu. Watu hawa hata hawakufika sehemu ya Raji', ambapo Banu Huzail waliwafikia na mapanga yasiyofunikwa na wakasema kwamba hatutaki kuwauwa. Bali, tunataka tupate fidia kutoka kwa watu wa Makka na tunaahidi kulinda uhai wenu. Hapo, Hazrat Marsad, Khalid na 'Asim (ra) wakasema hatuamini ahadi yenu. Hivyo, wote watatu wakatoa maisha yao wakipigana nao.

Hadhrat Abu Marsad bin Qannas bin Al-Hussain Ghanwi (ra), Alifariki katika mwaka wa kumi na mbili wa Hijra (Kuhamia Madina). Aliikubali Islam katika hatua zake za mwanzo mwanzo na alihamia Madina baada ya kuomba ruhusa kufanya hivyo. Mtume Mtukufu (saw) alifanya mkataba wa udugu kati yake na Hadhrat 'Ibada bin Samit (ra). Hadhrat Abu Marsad alikuwa pamoja na Mtume Mtukufu (saw) katika vita zote. Ana heshima katika Historia kutokana na tukio lifuatalo: Hadhrat Hatib bin Abi Baltah alipeleka barua kwa watu wa Makka kuwataarifu kisirisiri [juu ya mpango wa Mtume Mtukufu (saw)] kwa kutaka kuwalinda watoto wake kule. Allah alimfahamisha Mtume Mtukufu (saw) kuhusiana na hilo hivyo aliwapeleka wapiganaji watatu waliokuwa na farasi kumfuata mwanamke aliyekuwa anapeleka barua hiyo na wakamnyang'anya. Hadhrat Abu Marsad alikuwa ni mmoja wa wapiganaji hao watatu. Hadhrat Abu Marsad amesimulia Hadithi kutoka kwa Mtume Mtukufu (saw) ambayo imeandikwa kwenye Muslim. Anasema: "Nilimsikia Mtume Mtukufu (saw) akisema: 'Msikae kwenye makaburi na msisali kuyaelekea Makaburi." Alifariki wakati wa Ukhalifa wa Hadhrat Abu Bakr (ra) katika Hijra ya kumi na mbili akiwa na umri wa miaka sitini na sita.

Hadhrat Suleet bin Qais bin 'Amar (ra). Baada ya kuikubali Islam, wote wawili Sulaeet bin Qais na Hadhrat Abu Salma (ra) walivunjilia mbali masanamu ya Banu 'Adi bin Najjar. Hadhrat Sulaeet alishiriki katika vita vya Badr, Uhud, Khandaq na vita zote pamoja na Mtume Mtukufu (saw). Alifariki mwaka wa 14 wa Hijra wakati wa Ukhalifa wa hadhrat 'Umar (ra) katika vita vya Jisr huko Abi Ubaid.

Hadhrat mujazar bin Ziyaad alipata Ushahhid wakati wa Vita vya Uhud. Mujazr ilikuwa ni lakabu yake mbayo ina maana ya 'mtu wa miraba minne' Mtume Mtukufu aliweka undugu kati ya Hadhrat Majzar na 'Aaqil bin Buqair (ra). Hadhrat majzar alishiriki katika Vita vya Badr na Vita vya Uhud.

Hadhrat Hubbab bin munzar jumuh (ra) alikuwa ni sahaba aliyefariki wakati wa Ukhalifa wa Hadhrat 'Umar (ra). Alikuwa pamoja na mtume Mtukufu wakati wa Badr, Uhud, Khandaq na vita zote zingine. Alibaki thabiti bega kwa bega na Mtume Mtukufu (saw) wakati wa Vita vya Uhud.

Hadhrat Rifaa bin Raafi bin Malik bin Ujlan (ra) alikuwa ni miongoni mwa ma Ansari. Alikuwepo wakati wa bayati ya Uqbah na pia wakati wa Vita vya Badr, Vita vya Uhud, Vita ya Khandaq, Vita vya Rizwan na vita vingine vyote ambavyo Mtume Mtukufu (saw) alishiriki. Kaka zake wawili, Khallaad bin Raafi na Malik bin Raafi walishiriki katika Vita vya Badr.

Hadhrat Muaz anasimulia kwa maelezo ya baba yake (ra)- Hadhrat Rifaan bin Raafi, ambaye alishiriki katika Vita vya Badr- kwamba Hadhrat Jibrael (as) alimuuliza Mtume Mtukufu (saw) hisia zake kuhusu wale masahaba walioshiriki katika Vita vya Badr. Mtume Mtukufu (saw) alisema 'ni bora kupita Waislamu wote' au maneno yenye maana hiyo. Hadhrat Jibrael akajibu: "kwa namna hiyo hiyo, wale Malaika walioshiriki katika Vita vya Badr nao pia wana cheo cha juu kuliko wengine," Kuna maana ya kina ambamo Allah Alisema kwamba Alipeleka Malaika waliopigana. Lakini, haina maana kwamba malaika walikuwa wakipigana kwa mikuki kwa sababu na baadhi ya watu wanasimulia ati majeraha yaliyoletwa na Malaika kwa maadui yalikuwa yanaonekana tofauti kabisa na majeraha yaliyoletwa na Masahaba, hii sio kweli hata kidogo. Ukweli wa mambo ni kwamba waliviongoza vipaji vya kibinadamu na wakahakikisha vinatumika kwa namna iliyo bora kabisa. Yote haya yanapotokea kwa kuongozwa na Malaika basi ni sawa na kwamba ni wao ambao hasa wanapigana.

Ninapenda kusema kitu kuhusiana na Hotuba ya Ijumaa iliyopita na kufafanua zaidi kuhusiana na tukio fulani maalum. Ilielezwa kuhusiana na Hadhrat Amaar (ra) kwamba Hadhrat Amar bin Aas (ra) alionyesha huzuni kubwa na kuguswa wakati wa kifo chake kwa sababu alimsikia Mtume Mtukufu (saw) akisema Amaar atakuwa Shahiid kutokana na kundi la waasi. Lakini, watu wakauliza swali kwamba kama alikuwa miongoni mwa wale walioasi sasa kwa nini basi jina lake linapewa heshima kubwa kihivyo. Pia, Hadhrat Amir Muawiyah amepewa cheo cha kuonekana katika vitabu vya Jamaat. Kwanza, kuhusiana na vyeo vya Masahaba (ra), si juu yetu kuamua hatma ya Masahaba. Kutokana na kuelewa vibaya jambo lolote na kukosea hali hizo za kusikitisha zikatokea, jambo hili aachiwe Mungu Mwenyezi Pekee,, na Waislamu kwa kweli wamekumbana na matokeo ya hilo vilevile. Abu Zoha anasimulia kwamba Amar bin Shirajeel Abu Maisra, ambaye alikuwa miongoni mwa wanafunzi bora kabisa wa Hadhrat Abdullah bin Masuud, aliona katika njozi kwamba kulikuwa na bustani nzuri sana iliyojaa kijani ambamo kulikuwa na mahema machache. Moja lilikuwa la Hadhrat Amaar bin Yaasir, na kulikuwa na mahema mengine machache ambamo Dhulqaa pia alikuwemo mle. Abu Maisara akauliza hilo linawezekanaje kwani walipigana wao kwa wao. Kisha akasikia sauti ikisema, "Wamemkuta Mola wao Akiwa Msamehevu sana, na hivyo sasa wako pamoja." Hivyo, mambo haya sasa yamo kwa Mungu Mwenyezi. Sio jukumu letu kuyazungumzia mambo haya. Matukio haya yawe fundisho kwetu na badala ya kuyafuatilia, ni lazima tutafute njia za kujenga umoja. Siku moja nilitaja tukio lililosimuliwa na Hadhrat Musleh Maud (ra) ambalo lilimhusu Amir Muawiya. Kutokana na hilo mtu mmoja kutoka moja ya nchi za Kiarabu aliniandikia na akasema huyo alikuwa ni kiongozi wa kikundi cha wauwaji na waasi sasa kwa nini ninataja jina lake kwa heshima kiasi hicho. Kwa hiyo, simulizi hii ambamo njozi imetajwa ni jibu lenye kutosha kabisa kwamba Allah ni Msamehevu sana na Mwingi wa Rehema. Tujikite zaidi katika kurekebisha hali zetu na mambo yetu badala ya kutoa maoni juu yao. Ninamuomba Allah Atuwezeshe kubaki kama kitu kimoja na tubaki tumejengeka katika kuwa wamoja na tuwe mbele katika mambo mema. Amin

1958 - Najiunga na Ahmadiyya

Na Marehemu SEIF MUSSA SUNGU

Katika harakati za kuandika historia ya Ahmadiyya Tanzania nilikutana na Bwana Seif Musa aliyejiunganaAhmadiyyamwaka 1958. Maelezo yake yalikuwa ya kusisimua na nikamuomba atuandikie alivyojiunga. Makala haya ni matokeo ya ombi hilo – Mahmood Hamsin Mubiru

Mwaka 1950, niliota ndoto. Mtu mmoja mweupe mwenye ndevu nyingi akiniamsha akisema angalia kule, nikaona jua likichomoza upande wa Magharibi likiwa katika kiwango kama ya saa 1 hivi. Akaniambia "unasema leo jua linatoka Magharibi kuelekea Mashariki? Kiama tayari". Hapo nikaamka na moyo ukawa unanipigapiga sana. Mwaka 1956; Baba, mama na bibi yangu wakajiunga katika Jamaat Ahmadiyya. Ikawa baba yangu kuniagizia vitabu vidogo vidogo na magazeti. Kwa sababu wakati huo nilikuwa mtumishi katika Wizara ya Afya, kituo changu kilikuwa umbali wa kilometa 60 kutoka Nyipara. Kitabu kilichoniathiri mno kilikuwa *Safina Ya Nuhu*. Kitabu hiki nilikuwa nikikisoma na kurudiarudia, siku nyingine hunikosesha hata usingizi. Ikawa mara kwa mara zinanijia fikira kwamba iwapo nitakufa bila kujiunga Jamaat Ahmadiyya nitakwenda sema nini mbele ya Allah? Hatimaye mwaka 1958 nami nikaamua kujiunga katika Jamaat Ahmadiyya, moyo wangu ukapata utulivu. Kabla sijakaa vizuri likaanza kunizukia balaa! Mkasa wa kunyang'anywa wanawake ukaanza kuniandama; mke mmoja akachukuliwa na mmoja akagoma. Aliwaambia wazazi wake kwamba mimi sioni mabadiliko kwa mume wangu wala katika ibada huko msikitini. Mke huyu ambaye ndiye mama watoto wangu mpaka leo ametengana na Baba mzazi. Baba mzazi hakurudia hapo, alirudisha mahali niliyomwolea mwanawe, na zaidi akaomba na vile vyombo alivyomzawadia binti yakewakati akimwozesha kwangu. Baba huyu wa mke wangu aliyafanya haya mbele ya Mahakama ya mwanzo ya hapo Rusende. Huko kwenye sehemu yangu ya kazi likanitokea tokeo zito tena. Siku moja ikatokea nizungumze na Sheikh mkubwa kwa jina Sheikh Aliy bin Omar Makwega, wa baraza la mahakama la Msomeni. Ilikuwa miongoni mwa sehemu tatu (3) nilizokuwa nikizitembelea, yaani Msomeni, Muhoro na Ndundu. Baada ya kumpatia matibabu huyu Sheikh alianza kutoa matamshi ya kuilaumu Serikali:- Kusema kwamba, hii Serikali ya kikafiri inapoteza watu, ndipo nilipoanza kumjibu nikisema kwamba, shughuli za Dini na Serikali ni tofauti, kule kuacha kusema ukweli juu ya taadhima ya Dini ndiko ndiko kunakoleta uharibifu katika Dini. Huyu Sheikh mkewe alikuwa akicheza mila moja inaitwa "msondo". Katika mazungumzo huyu Sheikh alisema kucheza ngoma ya msondo ni mila ya wazee wetu. Nikamuuliza "wale walioacha mila zao wakati wa Mtume s.a.w wakafuata mafundisho ya Mtume waliitwaje? Akanijibu kwamba, hao walikuwa waumini. Nikamuuliza tena "wale waliokataa kufuata mila za Mtume waliitwaje? Akasinzia kutoa jawabu mara taramizi wake akachomoa kisu kutaka kunikata mimi ati kwa nini Sheikh nina mdodosa maswali mazito namna hiyo! Yule Sheikh alitoa amri kwa taramizi wake yule atupe kisu chini. Baada ya hapo wakakusanyika wazee na kumwandikia barua bwana DC wa wakati huo Mr. John Young, wakimweleza kwamba mganga huyu hatuna haja naye hapa, kwa sababu atapoteza watu kwa vile amekuwa Kadian. Bwana DC akapanga tarehe ya kukutana. Hali hii ikanitia wasiwasi sana kwa vile mimi mwenyewe si msomi kisha mchanga wa imani. Hivyo nikategemea anifuate Sheikh Swaleh Mbaruku, Bwana Maliki Mbungiro, hao wote sikuwapata. Lakini nikaupata msaada wa Allah kwa njia ya ajabu mno. Tarehe ilipofika, Bwana DC alifika akawaita wale wazee na walioandika barua pamoja na mimi nikasimama mbele ya Bwana DC. Swali "huyu mnamtambua kama nani hapa katika Baraza lenu? Wakajibu , ni mganga wetu. Yupo aliyekosa kutibiwa hapa kwa sababu huyu ni Kadian? Hapana, dawa na matibabu anatuhudumia kama kawaida. Sasa yeye hatakiwi kwa sababu ni Kadian sivyo? Ndio! Kesho yake Bwana DC hatakiwa kwa sababu ni Mkristo sawa? Kimyaa. Bwana DC akaendelea, ninyi ni kundi la watu fitina, na ni kama ni nyoka weusi tu. Tokeni mbele yangu. Siku nyingine nikiwagundua hivi nitawashughulikia ipasavyo, na ikilazimikahatakuchapwaviboko. Mkutano ukamalizika, na mimi sikuulizwa chochote katika kusanyiko hilo, nikaambiwa endelea na kazi yako. Hayo ndiyo yaliyoweza kunifika wakati nilipojiunga na Jamaat Ahmadiyyah miaka ya nyuma huku Rufiji.

Islam na Malezi Bora ya Watoto

Kutoka uk. 3

kwa wamchao (Mungu)." (Al-Furqaan: 75)

SALA

Tunapaswa kufundisha watoto wetu kumpenda Allah, kumwomba Allah na kumwamini Allah. Tunasoma katika Qur'an kwamba Hadhrati Nabii Ibrahimu (a.s) alikuwa akiomba kwamba: "***Mola wangu, Unijaalie niwe msimamisha Sala, na wazao wangu (pia); Mola wetu, na Upokee maombi yangu***." (Ibrahiim: 41)

Vilevile, Qur'an Tukufu inatufundisha: "Na uwaamuru ahali zako kusali, na uendelee kwa hayo; Hatukuombi riziki bali sisi Tuna waruzuku, na mwisho mwema ni kwa (washikao) ucha-Mungu." (Twaa haa: 133).

Muda wa kuwafundisha watoto wadogo ni mchache sana, hivyo fundisho la sala kwa watoto hutokea tu kwa kuwaona wazazi wao na wakubwa wengine wakiswali. Mwanzoni kabisa watoto wanaswali kwa kuiga wazazi wao. Mtukufu Mtume(s.a.w) alisema katika kipindi cha miaka 7 wazazi wanatakiwa kuwahimiza watoto wao kuswali. Katika umri wa miaka 10, watoto huvutwa na wenzao, hivyo wazazi wanatakiwa kuwaonya wanapoacha sala. Baada ya miaka 12 wazazi wawakumbushe watoto wao kusali. Ikiwa mzazi atashika ushauri huu basi hatojutia baadae.

Hadhrat Khalifatul Masihi wa IV(r.a) alikuwa akisema kwamba alijifunza kuswali sala zote kwa sababu mama yake alimsisitiza kusimamisha swala kwa wakati, iwe kwenye mikusanyiko au msikitini. Katika utoto wake mama yake alikuwa akimwamsha kutoka kitandani na alikuwa akimnyunyuzia maji kama alikuwa haamki wakati wa sala ya Alfajir. Kusimamisha sala tano kila siku inajenga nidhamu, uwajibikaji, na usafi kwa watoto.

Msisitizo wa kuzingatia sala kwa wakati ni muhimu sana tangu mwanzoni. Na kwa baadae kwa fadhila za Allah, ubora wa sala zao utaimarika, na mapenzi yao na Imani kwa mola wao utafuata. Na mwisho sawa na mafundisho ya Qur'an sala zao zitawaepusha na mambo mabaya na maovu. (Al-Ankabuti: 46).

MARAFIKI WA KWELI

Tunapaswa kuangalia marafiki wa watoto wetu. Qur'an Tukufu inatufundisha kwamba: "***kuweni pamoja na wasemao kweli***." (At-Tauba: 119). Kwahiyo kama sisi wazazi ni wa kweli na tunakaa na marafiki wa kweli, watoto wetu pia watafuata nyayo zetu. Inasemwa kwamba tabia ya mtu hujulikana kutokana na marafiki zake anaokaa nao. Zamani ilijulikana ni marafiki wale wa kimwili tu. Lakini sasa ni hata marafiki wale wakawaida (mitandao) tunaokuwa nao.

Sasa maendeleo ya sayansi na teknolojia, vishawishi vinapatikana kwa kutumia muda zaidi kwenye mitandao kuliko hata marafiki wale wa kimwili. Tunaweza kupoteza muda wetu mwingi kwenye TV, DVD, iPods, Myspace, Youtube, Facebook, Whatsapp, Instagram au badala ya kupoteza muda wetu tukawekeza katika kumkumbuka Allah, kukaa msikitini kwa lengo la kusoma, na kufanya majadiliano ya msingi, kuangalia MTA, na kuujua ukweli.

Ni juu yetu kutumia mitandao kwa kuzingatia mafundisho ya dini ya Islam, na kutafuta ukweli kwa njia za kusoma, na pia kufanya mahubiri, badala ya mabishano yasiyo ya msingi ambayo yanaweza kukufanya ushuke kiimani. Hivyo ishi na marafiki wazuri na tumia vizuri mitandao. Tukiwa kama wazazi tunapaswa kuwa ndio marafiki wa kwanza kwa watoto wetu. Kama tutaimarisha uhusiano na kuelewana, kuheshimiana, kupendana, uaminifu, na kujiamini kwa watoto wetu, hawatakuwa na haja ya kutafuta marafiki wengine sehemu nyingine.

Itaendelea toleo Lijalo



1. Hadija Yusuf Pinde wa Dutumi
2. Mahmood Mkeremi wa Mtwivila, Iringa
3. Hassani Kinywelo wa Mwananyamala
4. Shabani Rashid Magori wa Nyamuswa, Mara
5. Hawa Abdallah wa Kongowe, Dar es salaam

إِنَّا لِلّٰهِ وَإِنَّـا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ

Bustani ya Washairi

KUA UYAONE.

Kutoka toleo Lililopita

21. Koo linakukauka, kazi ya kujisifia
Jiangalie we Kaka, na muda unafifia
Mali zitaja ondoka, takuwa umefulia
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

22. Sisi sote ni ndugu, lazima kukumbushana
Hata ukane undugu, tumeungwa na Safina
Tabia hiyo bandugu, nami nasema hapana
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

23. Unajifanya wa moto, wala haushauriki
Wali moto mboga moto, mwendo mkiki mkiki
Ndugu taungua Moto!, kiburi kukimiliki
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

24. Hao wazee wakifa, shughuli imeshaisha
Waweza pata kifafa, Mali kizitaifisha
Nduguzo kina Hanifa, wataishi bila presha
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

25. Naweza pata kifafa, Mali kizitaifisha
Unavyopenda misifa, kwa watu kujionesha
Tayari wameshakufa, umebaki na bashasha
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

26. Umebaki na bashasha, maana litaka Mali
Wazazi wameegesha, wewe unawaza Mali
Kweli umeniangusha, ulivyokosa akili
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

27. Ngoja ukue uone, simaanishi ghorofa
Ujitume upambane, uje uzizibe nyufa
Fanya litekelemwene, uje upate maafa
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

28. Unajifanya mbabe, wenzako kuwakung'uta
Unatamba kwa utabe, Nguzo imara ukuta
Kama kweli ni mbabe, kapigane na Ukuta
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

29. Na una tabia mbaya, hata wazazi hawana
Na wala huoni haya, wazee kujibizana
Watu wanaimba kwaya, kikumbushwa unanuna
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

30. Ujana Maji ya Moto, kupoa hauchelewi
Usijione mtoto, kwa kufanya yasostawi
Takutana na msoto, pakuanza huelewi
Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

Abdallah S. Kalindima (K-Mtoto)
kalindimasenior@gmail.com

YULE

Yule ninani wahenga nawauliza
Analeta ufirauni vijana kuumiza
Anapoteza amani nuru yawagiza
Yule hasanani pateni kunijuza

Yule ni tafarani jamii anamaliza
amekosa soni fikra ameicharaza
kawatia sokoni utumwa kueneza
Yule Hasanani pateni kunijuza

Yule hayawani haki nawaeleza
Lilahi nishetani moto aupuliza
Vijana shikeni haya nayoeleza
Yule hasanani pateni kunijuza

Yule mhaini taifa kulipoteza
Kwetu nimgeni ufalme ajikweza
Vijana bagueni mapema fukuza
Yule hasanani pateni kunijuza

Yule mrubuni nyang'anyeni kipaza
Hatua chukueni rupango kumlaza
Dhamana nyimeni bakora charaza
Yule hasanani pateni kunijuza

Daudi Mkuty ***(Simba)***

SILIMU TASALIMIKA

1. Bismillah rahmani, rahimi mno hisani
Najikinga kwa manani, kutokana na shetani
Malumbano shairini, ni bora kwa waumini
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

2. Ni mzee mwenye dini, na kijana muumini
Ashusha yake matini, apinga kwa Qur-ani
Imani ake bayani, amtupia usoni
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

3. Maswali amesheheni, kajibu kiulaini
Si mbishi asilani, kwa suna kajalizani
Ajitafuta jamani, mengi yako mfukoni
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

4. Aliipinga imani, na dogo akabaini
Utume upo mwishoni, mbona bado mtamboni
Kaweka aya mezani, hee! Akacheka chini
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

5. Sura ya tano mwanzoni, kwani unataka nini
Ya nne kanakilini, kweli ipo Qur-ani
Wewe upo mabanoni, yeye yupo huzunini
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

6. Mungu katimiza dini, yeye atasema nini
Utume fika mwishoni, maswali mengi kichwani
Neema zote nguvuni, bwana nipe nafasini
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

7. Kutukamilia dini, sio mwisho wa shetani
Na watu wapo gizani, atawaokoa nani?
Mtume kabashirini, mtutia nguvu dini
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

8. Yamrudia kinywani, we husomi Qur-ani
Dogo unasema nini, huelewi tambuani
We mi nipo makini, waipinga Qur-ani
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

9. Sura ya nne jamani, aya yake ya sabini
Miongoni mwaumini, Nabii hakosekani
Ni fatadhi asilani, kitabu hakigongani
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

10. Neno ma'a changanyeni, maanaye miongoni
Mifano imesheheni, nitatoa wahidini
Maa'l muumini, ni kati ya waumini
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

11. Mzee ni piritoni, yey ni kama ndovuni
Ameza mate shingoni, maswali ni kifuani
Bado ye yupo kimyani, mwaga yake hadharani
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

12. Dini imetimiani, hakuna wema jamani
Au tu uongoni, ahadi yake manani
Mbona si kweli moyoni, msomi nakataani
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

13. Kweli nipo fikirani, wewe upo uzeeni
Khatama nnabiyyini, Ahzabu yarubaini
Maanaye ni mwishoni, mbona wapenda kubuni
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

14. Pete mbota maani, muhuri pia mwishoni
Ni mwisho mwajihoikani, kutupa yote pembeni
Kitabu cha rahmani, ki kweli hakibishani
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

15. Na tua mengi begani, kuwakinga na shetani
Aya ipo sababuni, kumlinda hatiani
Mtume wake makini, toka pale ghasiani
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

16. Mzembe yupo mwishoni, mbora yupo makini
Ipi yafaa jamani, kutoa mtu pangoni
Khatamannabiyyini, kweli si kitimishoni
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

17. A'RAAF kisomani, aya zake za mwanzoni
Watakuja rusuluni, toka kwetu miongoni
Aya kuzielezani, ndio lao jukumuni
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

18. Mzee yupo kichekoni, dogo hawaeleweni
Imam "kama" maani, hujaelewa jamani
Hiyo sio faradhini, bali kumbuka nduguni
Karibu Ahmadiyya, Ndugu tunawangojea

ZAID ABDALLAH MACHOMBE
MABIBO- DAR ES SALAAM

Litaendelea toleo lijalo

Mwaka 1953, Sheikh Kaluta Amri Abedi, alichapisha kitabu cha kwanza kinachoelezea sheria za kutunga mashairi. Al Ustaadh Khamisi Amani Khamisi Nyumaume, mmoja wa washairi mahiri wa Kiswahili alimpongeza Sheikh Amri Kaluta kwa kuimba;

Wallahi naapa Mungu,kushukuru sina budi,
Naapa kwa nia yangu, na kutia itikadi,
Nakiri kwa nia yangu, Amri kwetu kazidi,
K. Amri Abedi, fundi wa kwanza kutunga.

Sheikh Kaluta Amri Abedi alipokea pongezi hizo kwa kutoa utenzi ambao umebeba sifa za utenzi wa Kiswahili

1) Utungo wa "HEKO", Uliotunga,
Huna sokomoko, Huna bananga,
Kama fundi koko, Usiyejenga,
Utunzi ni wako, Jifurahie.

2) Na pendo la dhati, Linanisonga,
Lenye tashtiti, Kama kilanga,
La kinyamiti, Kititimanga,
Mawe na mchanga, Kitishie.

3) Na itunge siku, Yenye kutunga,
Ya mkukukuku, Wa kisomanga,
Tukae masiku, Huku twaringa,
Ringo la malenga, Tujiringie.

Dhuluma Ikizidi

Na dhuluma ikizidi
Ufanye kubwa juhudi
Ya kumuomba Wadudi
Kikombe kuepushia

Ongea na Mola wako
Ibadani ajue kilio chako
Ndiye Yeye mpokea vilio
Wote waombolezao

Iyonekayo ni hasara
Na isikupe harara
Rabi Anayo tijara
Ya thamani kuzidia

Sheikh Bashart-ur-rehman
Dar es salaam

Je Wajua?

Kwa Nini Mbu Haambukizi Virusi Vya UKIMWI?

Kumbuka kwamba; si UKIMWI bali ni VVU ambavyo husambaa kupitia damu, mama kwa mtoto na njia nyinginezo. Mbu hawawezi kusambaza VVU kwa sababu:

Kwanza kabisa, mbu anapokung'ata, hufyonza damu tumboni mwake. Tindikali tumboni mwake huvimeng'enya Virusi Vya UKIMWI (VVU). VVU huitaji seli zilizo maalum kama zile zinazopatikana kwa mwanadamu ili kujidurufu. Pia Virusi Vya UKIMWI havina uwezo wa kuwaambukiza wadudu wengine na kujizalisha ukilinganisha na vimelea vingine kama cha Malaria ambacho kinaweza kukua na kujidurufu tumboni mwa mbu, kisha kusafiri hadi kwenye kitunga mate ya mbu hatimaye kuendelea na mzunguko wake wa maisha kwa binadamu.



Pili, mkonga wa mbu haufanyi kazi kama sindano ya kawaida. Mrija unaotia mate kwa mtu ni tofauti na ule mbu anaotumia kufyonzea damu. Kwa hiyo damu tu huingia kwa mbu na mate ndiyo huingia kwa binadamu. Hata kama virusi visidhoofike au kufa papo hapo, haviwezi kutoka nje kwa sababu mbu hutumia mirija miwili tofauti kwa kufyonzea damu na wa kutilia mate yanayozuia damu yako kuganda na kutengeneza madonge wakati anainywa.

Jihadhari na Malaria

CHEMSHA BONGO



Kwenda Kulia
3. Msamehevu
5. Mkataba wa amani
8. Safina
12. Amani
14. Mleta wasiwasi
16. Diwani wa Nyamagana
17. Katu

Kwenda Chini
1. Mwezi wa pili
2. Mwezi mchanga
4. Mwenye nyumba dhaifu
6. Kuamini au kukubali ukweli
7. Silaha ya mwaminio
9. Vita ya nne ya Mtume
10. Malaika wa mvua
11. Wenyeji wa Madina
13. Zawadi ya thamani sana
15. Maono

Majibu Ya Chemsha Bongo la Toleo la Julai: *Hongereni mliopatia yote*

1. ALFAATIHA	6. JIBRIL	11. ABDUSSALAAM	15. SITA
2. UTUONGOZE	7. MUBARAK	12. UMRA	16. VIKTORIA
3. TAWAF	8. NIKAH	13. ALASIRI	17. TAUJIH
4. RUBAMAA	9. KADIANI	14. KHULA	
5. TALAKA	10. AMINA		

Tunawapongeza wafuatao waliotutumia majibu ya Chemsha Bongo lililopita. *Jazak Allah Khaira*

Rukia Juma KImanda - Mengwa, DSM
Naiphath Chikurupi Kawinga - Safina, DSM
Khadija Ch. KAwinga - Safina, DSM
Muniba HArun Lundo - Kitonga, DSM

TAFUTA MANENO

Kuna maneno 26 katika jedwali hapa chini. Yatafute kwa kuyazungushia na Penseli
Kumbuka: Maneno yote ni ya Kiswahili tu

U	H	Q	H	N	N	R	E	D	I	O	P	X	P	H
J	Q	D	T	Q	C	J	R	Q	Q	F	O	T	C	E
N	J	B	H	P	N	M	T	Z	U	D	P	M	S	K
N	R	M	A	A	P	B	B	A	N	R	A	M	H	O
K	A	B	H	H	T	L	P	E	L	Y	A	M	A	S
A	N	S	K	U	L	I	P	M	I	A	L	N	I	H
D	K	X	A	K	H	U	H	U	D	A	K	Y	R	A
I	A	H	R	B	X	A	M	B	D	T	H	A	I	H
A	B	R	N	J	A	U	B	A	N	A	K	R	K	I
N	U	Z	E	M	J	W	B	E	W	D	D	I	M	D
I	T	K	U	F	C	I	T	V	S	A	E	R	N	V
R	K	H	T	U	K	U	F	U	B	H	C	P	J	T
D	U	A	X	T	K	K	C	L	S	T	I	D	L	P
T	W	F	M	Z	U	L	I	M	W	E	N	G	U	E
N	R	T	I	J	A	R	A	Z	C	C	P	H	C	P

Ukhalifa Ndio Taa ya Islam

Na **Bwana Jumanne Rajabu**
Morogoro

Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya ilianzishwa 1889 na muanzilishi wake Masih Aliyeahidiwa wa Mtukufu Mtume s.a.w. Seyidna Ahmad a.s. Uongozi wa Ukhalifa katika Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya ulianzishwa 27-5-1908 baada ya kifo cha muanzilishi wake Masihi aliyeahidiwa Sayidna Ahmad a.s. Khalifa wa kwanza alikuwa Hafidh Alhaji Maulana Nur-ud-din tokea 1908 -1914. Khalifa wa pili alikuwa ni Hadhrat Sahibzada Mirza Bashir –ud-din Mahmood Ahmad, mwana aliyeahidiwa, tokea 1914 – 1965. Khalifa wa tatu Hadhrat Hafiz Mirza Nasir Ahmad tokea 1965 – 1982.

Khalifa wa nne Sahibzada Mirza Tahir Ahmad tokea 1982 -2003. Khalifa wa tano Sahibzada Mirza Masroor Ahmad tokea 2003 hadi sasa. Mpaka 27/5/2008 uongozi wa Ukhalifa katika Jumuiyya Ahmadiyya ulikwishafikia karne moja na ushekhe wa uongozi wake.

Wapinzani wa Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya ni mshahidi juu ya jambo hili duniani kote. Tokea kuanzishwa kwa Jumuiya Ahmadiyya wapinzani wa Jumuiya wamekuwa wakitoa shutuma nyingi mbalimbali kwa kuibeza Jumuiya pamoja na viongozi wake kwa kutamka hadharani kuwa Jumuiya gani hii ambayo waumini wake hawajai hata kiganja kimoja cha mkono? Ukweli wa shutuma zote hizi za wapinzani wameshindwa kuelewa jambo moja kubwa na muhimu sana ambalo hawana elimu nalo, nalo ni hili – uamuzi wa kuongeza au kupunguza kitu, viko juu ya Allah mwenyewe hufanya mbegu yake ikue, na wakati anapokuwa katika umbile la mbegu moja, watu huwa wanashangaa na kujiuliza ni kwa jinsi gani idadi yake itafikia maaelfu. Ifahamike kuwa jibu lake sahihi ni kwamba Allah pekee ndiye mwenye uwezo wote anafanya mbegu ikue. Naamini kwa maelezo haya wapinzani wetu watakuwa wamepata somo ambalo kwa umbumbumbu wao walikuwa hawajui.


Jumanne Rajabu sahib Mwandishi wa Makala

Inafaa ikumbukwe kuwa Seyidna Ahmad a.s. alipoanzisha Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya alikuwa mtu mmoja peke yake, na hakuwa na dalili hata ile ndogo kuwa angepata wafuasi wa kumkubali na kumfuata. Watu wachache walipoanza kumkubali na kumfuata Seyidna Ahmad a.s. watu hao waliitwa watu wachache wapumbavu. Wakati idadi ya wafuasi wake ilipokuwa inaongezeka na kufikia maelfu. Ikasemwa kuwa kumbe hawa watu wenye akili zao timamu na wajanja nao pia wanaweza kudanganywa. Hata hivyo ilifikiriwa kuwa Jamaat haiwezi kukua kufikia mamilioni. Wapinzani wa Jumuiya kama ilivyo hulka yao wanashindwa kabisa kufikiria ukweli kwamba jinsi Jamaat ilivyoanza kutoka mtu mmoja mmoja mpaka watu kumi na kutoka watu kumi na kufikia watu mamia, na kutokea watu mamia hadi kufikia watu maelf mpaka mamilioni. Ndani ya karne moja ya uongozi wa Ukhalifa, Jumuiya ya Ahmadiyya imekwisha enea katika nchi zaidi ya 200 duniani kote, ushindi ambao haujafikiwa na wala hautafikiwa na dhehebu lolote la Islam.

Jumuiya Ahmadiyya inaendelea kuandika maelfu ya vitabu vya dini ya Islamu, magezeti na vipeperushi kwa nia ya kuendeleza dini ya Islamu. Ushindi huu wote umepatikana na utaendelea kupatikana ndani ya Jumuiya chini ya ungozi wa Khalifa matokeo yake ni sawa na HAKUNA. Ukweli wa jambo hili Allah amekwisha lisema ndani ya kitabu chake Qurani Tukufu Sura 24.56 Isimeyo:-

Allah amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri bilashaka atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya Makhalifa wale wa kabla yao, na kwayakini atawaimarishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia Amani baada ya hofu yao, wataniabu hawatanishirikisha na chochote, na atakaekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri.

TAMBIO: Ifahamike wazi wazi kuwa wapinzani wa Jumuiya Ahmadiyya kamwe hawataweza kuzuia maendeleo ya kiroho ya Jumuiya Ahmadiyya mpaka siku ya kiyama. Katika karne hii ya pili ya uongozi wa Ukhalifa Jumuiya ya Ahmadiyya ni karne ya pili ya ushindi wa dini ya Islam. Huu ndio wito kwenu nyinyi wapinzani wetu kuharakisha kujiunga katika Jumuiya ya Masihi Aliye wa Mtume s.a.w. Seyidna Ahmad a.s.

MWISHO: MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Mkutano Wa Amani Wafana Kagenyi

Na **Mwandishi Wetu**
Kagera

Katika kuendeleza mwito wa kiongozi Mtukufu wa Jamaat Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) wa kueneza ujumbe wa amani, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jamaat Ahmadiyya Sheikh Tahir Mahmood Chaundry ambaye alizuru kanda ya Ziwa, amehutubia mkutano wa amani kijiji cha Kagenyi. Mkutano huo uliohudhuriwa na wananchi wa dini mbalimbali ulivutiwa na hotuba aliyotoa Amir Sahib.

Akiwahutubia waliohudhuria Amir sahib alisema, amani ndiyo msingi wa maendeleo ya kimwili na kiroho katika jamii yeyote.


Wahudhuriaji wakifuatilia kwa makini mkutano wa amani

Maendeleo yeyote hayawezi kuja bila kuzingatia utamaduni wa kuheshimu amani.

Mkutano huo wa kwanza mkoa wa Kagera kuhudhuriwa na Amir Sahib Tanzania, pia ulihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa Mh. Shaabani Ilangu Lissu na Mbunge wa Jimbo la Kyerwa Mh. Innocent Bilakwate.


Amir sahib akipokewa na wenyeji wake

Akizungumza katika Mkutano huo Mkuu wa Wilaya alisema, kuchezea amani ni sawa na kuchezea sharubu za simba na kuwataka wananchi kuitunza amani tuliyonayo.

Mkuu wa Wilaya ambaye amesema anaijua Ahmadiyya toka mwaka 1974 alipokuwa anasoma kidato cha kwanza mjini Tabora. Aliendelea kusema katika hotuba yake ya kusisimua.

Mkuu wa wilaya alisema anafahamu jinsi Ahmadiyya ilivyosaidia kuondoa fikra za uchawi na ushirikina kwenye mikoa ya Simiyu na Shinyanga na kuomba kufanya hivyo wilayani kwake.

Wakati wa mvua ya mawe iliyoikumba baadhi ya vijiji vya Wilaya yake, Kagenyi ilikuwa ndiyo kijiji cha mwanzo kujitokeza kusaidia waathirika. Sasa ndiyo anajua siri yake, alitanabaisha Mkuu wa Wilaya.

Akitoa nasaha zake katika Mkutano huo, Mbunge wa Jimbo Mh. Innocent Bilakwate alisema kuwa Jamaat Ahmadiyya ni mfano wa kuigwa katika makundi yote ya imani yaliyomo jimboni mwake na kuitaka Jumuiya


Mh Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa Mh Shaabani Ilangu Lissu (kushoto) na Mbunge wa Jimbo la Kagenyi Mh Innocent Bilakwate wakitoa nasaha zao katika mkutano wa amani



Wenyeji wa mkutano pamoja na Amir sahib na viongozi wa kisiasa

iendelee kudumu kwa kufanya mikutano ya amani kama hii.

Mkutano huo ulifungwa na Amir Sahib, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry kwa maombi na kupata Chakula cha pamoja na wageni waalikwa toka sehemu mbalimbali.

Studio ya MTA Tanzania Yakamilika, Redio Ahmadiyya Mtwara Yapasua Anga

Na **Pazi Mazongera**

Katika kuonyesha kushika kasi ya aina yake katika uwanja wa mahubiri kupitia vyombo vya habari, Mitambo ya studio ya MTA (Muslim Television Ahmadiyya) iliyopo Mkoani Morogoro nchini Tanzania imemalizika matengenezo yake. Studio hiyo ya kisasa ambayo ina uwezo kurekodi na kutuma matukio mbalimbali yatakayotokea Tanzania na nchi za jirani kama Kenya, Uganda,Rwanda, Burundi, Msumbiji, Zambia, Malawi na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo.



Amir sahib Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry (kulia) akiwa ndani ya Studio za MTA Tanzania mjini Morogoro

Akitembelea Studio hizo mjini Morogoro Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundry akiwa na mgeni wake Sheikh Javed Muhammad ambaye ni Amir na Mbashiri Mkuu wa Jamaat Ahmadiyya nchini Zambia, alionyesha furaha yake na kumshukuru Allah kwa kumalizika kwa ujenzi na ufungaji wa vifaa vya kisasa katika Studio hiyo ambayo ujenzi ulichukua takribani miaka miwili sasa.

Studio hiyo inayosimamiwa na Sheikh Asif Mahmood Butt ambaye ni Mbashiri wa Mkoa wa Morogoro chini ya usimamizi wa Amir Sahib Tanzania, itakuwa inaratibu shughuli zote zinazohusu MTA-Africa na MTA International ambazo matangazo yake yanarushwa moja kwa moja duniani kwa satelaiti toka nchini Uingereza.

Kwa sasa na siku zijazo tutaweza kurekodi wenyewe vipindi kwa kutumia Studio hii na kuvituma kwa kurushwa kwenye ltuninga, tutaweza pia kuangalia matukio mbalimbali yanayotokea nchini kwa uzuri zaidi, Alisema Amir Sahib huku akiungwa mkono na mgeni wake.

Aidha, katika tukio lingine la aina yake kutokea kwa Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Jamaat Ahmadiyya Tanzania kwa mara ya kwanza katika historia imepata kibali cha kurusha kwa majaribio Redio Ahmadiyya katika Mkoa wa Mtwara na tayari iko hewani kwa takribani mwezi mmoja sasa. Nakumbuka Mahmood Hamsin Mubiru alitumwa na Sheikh Muhammad Munawwar, Amir na Mbashiri Mkuu wa siku hizo kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Habari na Utangazaji kuomba fursa ya kutoa mafunzo ya dini tukufu ya Islam kupitia Redio Tanzania. Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari na Utangazaji wa wakati huo ndugu Paulo Sozigwa alisema: “mkitaka kutumia redio mkaombe kibali BAKWATA”. Sheikh Muhammad Munawwar Chaudhry alifuta machozi na akasema “Insha Allah, Allah Atatupatia redio yetu”, Alhamdulillah maombi yamepokelewa.



Sheikh Abdulrahman Ame akijaribu mitambo ya Redio Ahmadiyya Mtwara

Redio hiyo iitwayo FM 99.3 Redio Ahmadiyya Mtwara, inatarajiwa kukonga nyoyo za watu katika kutoa elimu sahihi ya dini Tukufu ya Islam kwa mujibu wa Qur’an Tukufu na Sunna za Mtume Mtukufu Muhammad saw.

Redio hiyo inayorushwa katika masafa ya FM, inatarajiwa kuwa kichocheo cha amani na ustawi katika nchi na kutoa fursa za kimaendeleo ya kiimani kwa wanadamu na kumcha Allah vizuri zaidi.

Katika kipindi hiki cha majaribio itasomwa Qu’ran Tukufu na Mashairi mbalimbali ya kidini wakati utaratibu wa kupata kibali cha kudumu zinafuatiliwa ili kuwa na vipindi kwa utaratibu sawa na mamlaka ya Serikali itakavyoona inafaa.

“Nitaufikisha Ujumbe Wako Pembe Zote za Dunia”, huu ni ufunuo wa Masihi na Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Ahmadiyya duniani, Seydna Ahmad (as) ambaye wakati anapata Wahyi huu dahari ya miaka iliyopita, hakuwa mwenye kujua njia zitakazotumika baadaye za kiteknolojia katika kufikisha ujumbe wa Allah.



Amir sahib Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry na mgeni wake Sheikh Javed Muhammad kutoka Zambia wakikagua studio za MTA Tanzania mjini Morogoro hivi karibuni

Kwa fadhila za Allah, ikaja MTA International, MTA-Arabia, MTA- Africa na kwa Sasa vituo vingi vya Redio, Studio, Magazeti na majarida mbalimbali, Intaneti ambamo kuna You-Tube, Instagram, emails, Twitter na mtandao wa Whatsapp umeleta mageuzi makubwa ya kimawasiliano na mahubiri katika ulimwengu wa sasa.

Redio hiyo inayorusha kupitia kwenye masafa ya FM, inasimamiwa na Sheikh Ali Dino Tahir ambaye ni Mbashiri wa Mikoa ya Lindi na Mtwara chini ya uangalizi wa Amir Sahib Tanzania kwa hivi sasa iko hewani na inasomwa Qur’an Tukufu na Mashairi ambayo imekuwa kivutio cha wasikilizaji wengi wa Mkoa wa Mtwara na maeneo ya jirani.

Ni matarajio ya Watanzania wote kuwa, vyombo hivi vya habari vitatumika kwa ajili ya kumcha Mungu na kuwaunganisha wanadamu na Mola wao na kuwa raia wema ili kufikia malengo ya kuumbwa kwetu.

MATUKIO KATIKA PICHA



Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Akifungua kituo cha basi cha Msamvu mjini Morogoro pamoja na viongozi wa dini mbalimbali



Amir na Mbashiri Mkuu pamoja Wanajamat wa Bugimbagu baada ya ufunguzi wa Masjid Baitul Mumin



Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Anthon Mtaka akiwa na ujumbe wa Jamaat ofisini kwake



Banda la kuita watu kwenye kheri lilibuniwa na Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania lililopo Kariakoo jijni Dar es salaam



Amir sahib akiwa na mgeni Sheikh Javed Muhammad pamoja na Mkuu wa Chuo cha Jamia na Wahadhiri wengine wa Jamia Ahmadiyya Tanzania



Amir sahib akisalimiana na Mkuu wa Wilaya ya Itilima Benson Kilangi ofisini kwake



Nasrat wa Nungwe wakighani shairi wakati wa ufunguzi wa msikiti Nungwe, Geita



Amir sahib na wanajamaat wakiwa na viongozi wa Wilaya ya Geita walipowatembelea kabla ya ufunguzi wa msikiti

Watu Walio Bora Kabisa

Inatoka uk 12

Mtukufu (saw) alitoa zaidi na akaonyesha wema wake. Tukio lote hili linatosheleza kuwa jibu kwa tuhuma zinazotolewa dhidi ya Mtume Mtukufu (saw) kuhusiana na wakeze kwamba, Mungu Apishie mbali, alikuwa anapenda wanawake warembo.
Hadhrat Abu Usaid alikuwa akisema kwamba chochote kinachoombwa kutoka kwa Mtume Mtukufu (saw), kamwe hakubeza au kukataa.
Sahaba mwingine ni Hadhrat Abdullah bin Abdil Asad. Jina lake lilikuwa ni Abdullah na alijulikana kama Abu Salmah. Mama yake alikuwa ni Barrah bint Abdil Muttalib. Alikuwa ni binamu wa Mtume Mtukufu (saw) na alikuwa ndugu wa kulea wa Mtume Mtukufu (saw) na pia Hadhrat Hamza. Alinyonyeshwa na Sobiah, mtumishi wa Abu Lahab. Mwanzoni alimuoa Ummi Salmah. Kuhusiana na hili Hadhrat Mirza Bashir Ahmad pia anaandika katika Seerat Khatamun Nabiyyin kwamba Abu Salmah bin Abdil Asad alikuwa ni ndugu wa kulea wa Mtume Mtukufu (saw) na alikuwa ni wa kabila la Banu Makhzoom. Baada ya kifo chake, mke wake Ummi Salmah aliolewa na Mtume Mtukufu (saw). Hadhrat Abdullah bin Abdil Asad alikuwa ni miongoni mwa watu wa mwanzo kuikubali Islam.
Abdullah bin Abdil Asad na mke wake Ummi Salmah (ra) walikuwa ni miongoni mwa wale katika uhamiaji wa kwanza kwenda Uhabeshi. Baada ya kurudi Makka kutoka Uhabeshi walihamia Madina. Ibn Ishaaq anasimulia kwamba wakati Abu Salma aliporudi kutokea Uhabeshi na aliomba hifadhi ya Hadhrat Abu Talib, watu wachache wa Banu Makhzoom walimtembelea Abu Talib na wakauliza, "Umempa hifadhi mpwa wako Muhammad, lakini kwa nini umempa hifadhi ndugu yetu Abu Salma?" Abu Talib akajibu, "Ameomba hifadhi kwangu naye pia ni mpwa wangu (mtoto wa kiume wa dada). Kama nisingempa hifadhi mpwa wangu [mtume Mtukufu (saw)] basi nisingempa hifadhi mpwa wangu mwingine."
Abuu Salamah bin 'Abdul-Asad (ra) alipata majeraha wakati wa vita vya Uhud na kisha alilazimika kwenda vitani kukisambaratisha kikundi cha watu ambao walikuwa wanawachochea watu wa mkoa wao kupigana vita dhidi ya Mtume Mtukufu (saw). Kutokana na shida za safari hiyo, majeraha aliyoyapata Abuu Salamah (ra) kule Uhud, ambayo kiasi fulani yalikuwa yanaonekana yamepona wakati huo, yalianza kuuma tena. Ingawa alipata matibabu, majeraha yaliendelea kuzidi, na hatimaye kwa majeraha haya haya, Sahaba mwaminifu na mwasisi wa Mtume Mtukufu (saw), ambaye alikuwa pia ndugu wa kulea wa Mtume Mtukufu (saw) akafariki. Abu Salma (ra) alipofariki, Mtume Mtukufu (saw) aliyafunga macho yake yaliyokuwa wazi na akaomba baada ya kifo chake kwamba "Ee Allah, Mtendee Abu Salmah kwa usamehevu na Unyanyue cheo chake miongoni mwa watu waliongoka, Uwe Mlinzi wa warithi aliowaacha nyuma. Ee' Mola wa walimwengu wote! Tusamehe na sisi pia." katika Hadithi nyingine imesimuliwa kwamba katika dakika za mwisho za maisha yake, Hadhrat Abu Salmah (ra) aliomba, "Ee Allah! Umpate mtu mbora kabisa wa badala yangu ambaye ataiangalia familia yangu." Hivyo, dua hii ilikubaliwa na Mtume Mtukufu (saw) akamuoa Ummi Salma (ra).
Hadhrat Ummi Salma (ra) anasema, "Wakati Abu Salma (ra) alipofariki Shahid, niliomba – ingawa moyo wangu haukutaka kutamka dua hii – kwamba 'Ee Allah! nijaalie mwingine mbadala wa Abu Salma (ra)" Kisha nikasema moyoni nani anaweza kuwa mwema zaidi ya Abu Salma (ra); alikuwa na sifa hii na ile. Kwa maneno mengine, alikuwa na sifa na tabia nyingi nzuri, lakini bado niliomba dua hiyo." Eda ya Hadhrat Ummi Salma ilipoisha, alipokea ujumbe kutoka kwa Mtukufu Mtume (saw) ukimuomba mkono wa ndoa.
Mtume Mtukufu (saw) alipopeleka ombi la ndoa kwa Ummi Salamah (ra), kwa namna fulani alikataa akitoa sababu ya shida kadhaa na akaomba radhi kwa kusema, "nimeisha kuwa mzee na siwezi tena kuzaa watoto". Lakini, mwishoni akakubali. Mtoto wake wa kiume akawa walii wake na kamuoza kwa Mtume Mtukufu (saw). Kama ilivyokwisha semwa, Ummi Salamah (ra) alikuwa ni mwanamke mwenye hadhi ya kipekee na zaidi ya kuwa na akili sana na shapu, alikuwa na daraja la juu katika utiifu na imani. Hadhrat Ummi Salamah (ra) alijua kusoma pia, na alifanya kazi kubwa ya kuwaelimisha na kuwafunza wanawake wa Kiislamu. Masimulizi mengi na Hadithi zimesimuliwa na yeye katika vitabu vya Hadithi, na kwa muktadha huu anakuwa wa pili miongoni mwa wake wa Mtume Mtukufu (saw) na wa kumi na mbili miongoni mwa masahaba kwa ujumla (kujumlisha wote wake kwa waume).
Hivyo, hivi ndivyo walivyokuwa Masahaba (ra). Ninamuomba Allah Mwenyezi Aendelee zaidi na zaidi kunyanyua vyeo vyao vya juu na pia Atuwezeshe nasi kushika matendo yao mema, Amin.
Sasa nitaelezea kwa urefu kiasi fulani habari za watu wachache ambao wamefariki hivi karibuni na pia nitasalisha jeneza ghaib kwa ajili yao.
Wa kwanza ni Raja Naseer Ahmad Nasir, ambaye alifanya kazi akiwa amejitolea wakfu maisha yake akiwa Mbashiri wa Jamaat. Hapo kabla pia alifanya kazi kama Nazir Islaah o Irshaad Markaziyya. Alifariki tarehe 6 Julai 2018 katika Taaisi ya Moyo ya Tahir huko Rabwah akiwa na umri wa miaka 80. Inna liLlahi wa inna ilaihi raajiuun. Baada ya kuhitimu katika Jamia Ahmadiyya, alipata fursa ya kuitumikia Jamaat kwa miaka 47.
Alikuwa na imani kubwa kwa Mungu Mwenyezi na alikuwa makini katika dua zake na sala. Mtoto wake wa kiume ameandika kwamba wakati walipokuwa wakiishi huko Bangladesh, moto uliwakanakaribuulikuwauzifikie nyumba za Waahmadiyya. Hapo akaomba, "Ee Allah! Masihi Wako amesema, '[usinitishe na moto,] kwani moto ni mtumishi wangu na pia mtumishi wa watumishi wangu' hivyo utuokoe na moto." Anasimulia kwamba moto ukazikaribia nyumba na hata miale ya moto ilikuwa inagusa kona ya moja kati ya nyumba hizo, lakini ukaishia pale na haukutapakaa zaidi na nyumba za Wahmadiyya zikaokolewa.
Alikuwa na hamu kubwa katika kuisoma Qur'an Tukufu. Mtoto wake wa kiume ameandika kwamba baba yake alipania kukamilisha kuisoma Qur'an angani na majini. Alimaliza Qur'an mara nyingi ardhini. Hivyo, alipata fursa ya kumaliza kuisoma Qur'an Tukufu akiwa anasafiri baharini. Safari ya angani haikuwa ndefu vya kutosha lakini hata hivyo alitumia muda mwingi wakati akiwa anasafiri ndani ya ndege, alikuwa akiisoma Qur'an Tukufu. Mtoto wake wa kiume, ambaye amejitolea wakfu maisha yake na ambaye kwa sasa anafanya kazi katika idara ya Wakalat-e-Tasniif, Bwana Raja Ataul Manan, anasema kwamba baba yao daima alikuwa anawashauri kuhusu vitu viwili; kutofanya Shirk kamwe na daima kushikamana na Taasisi ya Ukhalifa wa Kiahmadiyya kwa hali yoyote. Yeye mwenyewe pia daima alishikamana na kanuni hizi mbili.
Sambamba na hili kuna sala ya jeneza ya mashahidi wawili, ambao ingawa hawakuuwawa kwa ajili ya Jamaat, lakini ujambazi ulifayika katika duka lao na wezi wakawapiga risasi na matokeo yake wakafa mashahidi. Mmoja wao ni Mubeen Ahmad Sahib, mtoto wa Mehbuub Ahmad Sahib, na mwingine ni Muhammad Zafrulla Sahib, mtoto wa Liaqat Ali Sahib. Tarehe 7 Julai 2018 kwenye majira ya takriban saa tisa alasiri, kwenye eneo la viwanda la Korangi huko Karachi, majambazi yenye silaha yaliyafyatulia risasi Khuddam watatu; majina yao ni Mubeen Ahmad Sahib, mtoto wa Mehbuub Ahmad Sahib, Zafrullah Sahib na Muhammad Nasrullah Sahib. Matokeo yake Mubeen Ahmad Sahib na Zafrullah Sahib waliuwawa. Inna liLlaahi wa Inna iaiHi raajiuun. Majambazi hayo yenye silaha yalitaka kukomba duka lao la vifaa vya kielektroniki. Kwa kuwa waliwazuia basi wakawafyatulia risasi na kuwauwa.
Mubeen Ahmad Sahib alikuwa anasomea Shahada ya Sanaa na katika umri wa kifo chake cha Ushahhid alikuwa na umri wa miaka 20. Mubeen Ahmad Sahib alikuwa na sifa nyingi nzuri. Alikuwa mstahmilivu sana, na alikuwa anadhibiti hasira na alikuwa mwenye nguvu. Alikuwa akisali sala tano kwa kudumu na alimtendea kila mtu nyumbni kwake kwa upendo na heshima. Marehemu alikuwa akishiriki kikamilifu katika shughuli za Jamaat na alikuwa ni khaddim hai. Ilipokuwa inabidi aache kazi zake binafsi ili kufanya kazi za Jamaat alikuwa akifanya hivyo bila kusita. Marehemu alijiunga na Wassiyyat na alipewa namba yake ya kumbukumbu. Wassiyyat wake utakubaliwa, InshaAllah. Alikuwa na uhusiano mzuri na majirani zake wote. Kila mmoja amelisema hilo si wazee si vijana. Mubeen Ahmad Sahib alikuwa na undugu na mtu wa pili aliyekufa kishahhid katika tukio hili, Muhammad Zafrullah Sahib, kupitia kwa shangazi yake. Pamoja na baba yake, Bwana Mehbuub Ahmad Sahib na mama yake Bi Amatul Hafeez Begum Sahiba, ameacha madada zake wawili; Mubeena Mehbuub mwenye umri wa miaka 23 na Kinzah Mehbuub mwenye umri wa miaka 16 na mdogo wake mmoja Amiin Ahmad mwenye umri wa miaka 13.
Shahidi wa pili ambaye sala yake ya jeneza pia nitaiongoza ni Muhammad Zafrullah Sahib, mtoto wa kiume wa Liaqat Ali Sahib. Katika tukio hili alipigwa risasi tatu ambazo ziliharibu vibaya mafigo yake yote mawili. Operesheni yake ilifanikiwa, lakini afya yake ikadhoofika tena. Madaktari wakaamua kumfanyia operesheni nyingine, lakini, akafariki usiku uliopita. Inna liLaahi wa inailaii raajiuun. Ahmadiyya pia iliingia katika familia yake kwa kupitia baba wa babu yake Bwana Ghulam Diin Sahib, ambaye alikuwa anatokea wilaya ya Gurdaspur na alifanya kazi katika ardhi iliyokuwa inamilikiwa na Sahaba mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa (as), Hadhrat Abdul Aziz Patvari. Siku moja alikwenda naye Qadian na baada ya kuonana na Masihi Aliyeahidiwa (as) akajaza baiati.
Marehemu Muhammad Zafrullah Sahib alizaliwa mwezi wa kumi mwaka 1993 huko Karachi. Alikuwa ni khaddim mcheshi na mwenye khulka njema, ambaye daima alikuwa na tabasamu kwenye uso wake. Marehemu alikuwa akifanya sana kazi za Jamaat na alikuwemo kwenye idara mbali mbali katika Khuddamul Ahmadiyya. Kwa Baraka za Allah alikuwa ni Muusi na alikuwa na umri wa miaka 25 alipouwawa kishahhid. Amemuacha baba yake, Liaqat Ali Sahib, mama yake Naseera Begum Sahiba na ndugu watano; Wajahat Ahmad mwenye umri wa miaka 33, Mansoor Ahmad mwenye umri wa miaka 31, Mustenser Ahmad, miaka 28, Shuja Ahmad, miaka 27 na Hadiz Nasrullah, ambaye sasa hivi yuko hospitali akifanyiwa upasuaji. Ninamuomba Allah Amjaalie kupona haraka na Ampe afya kamili, Amin. Ninamuomba Anyanyue vyeo vya marehemu na Awajallie famila zao uimara Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SHAWW - DH. QAD 1439 AH | AGOSTI 2018 | ZAHOOR 1397 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Sa'd bin Abi Waqqas r.a. aliyesema kwamba nilimsikia Mjumbe wa Allah s.a.w. akisema: Allah Humpenda mtu ambaye ni mcha-mungu, mkwasi na apendaye kuishi katika upweke. (Muslim)

Watu Walio Bora Kabisa

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 13 Julai 2018, baada ya usomaji wa Tashahhud, Ta'wwuz na Surat Al- Fatihah, Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema: leo nitazungumzia zaidi juu ya Masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w). Wa kwanza ni Hadhrat Abu Usaid Maalik bin Rabia Sa'idi. Hadhrat Maalik bin Rabia r.a alikuwa anajulikana vizuri kama Abu Said. Baadhi wanasema jina lake lilikuwa ni Bilal bin Rabia. Alikuwa anatokana na watu wa Banu Sa'da ambalo ni tawi la kabila la Khazraj. Hadhrat Abu Usaid Maalik bin Rabia alikuwa ni mfupi kwa kimo. Nywele zake na ndevu zilikuwa na mvi, lakini alikuwa na nywele zilizoenea kichwani kwake. Katika wakati wake wa uzee alipoteza uwezo wake wa kuona na alifariki katika Hijri ya 60 kipindi cha Muawiyyah akiwa na umri wa miaka 75. Alikuwa ni mtu wa mwisho kufariki miongoni mwa Maansar walioshiriki katika vita vya Badr. Hadhrat Abu Usaid aliungana na Mtukufu Mtume(s.a.w) katika vita vya Badr, Uhud, Khandaq na vita vingine za baadae. Alichukua uongozi wa Banu Sa'da wakati wa ushindi wa Makka.

Hadhrat Sulaiman bin Yassir r.a anasimulia kuwa kabla ya kuuwawa kwa Hazrat Uthman r.a, Hadhrat Abu Usaid Sa'di alipoteza uwezo wake wa kuona na macho yake yalikuwa yamepofuka moja kwa moja. Hivyo, kutokana na hili alikuwa akisema, " Namshuru Allah kwa kunipa uwezo wa kuona kipindi cha uhai wa Mtukufu Mtume(s.a.w) na kuniwezesha kuona Baraka zote hizi. Lakini zaidi, wakati Allah Mtukufu alipoamua kuwaweka watu kwenye majaribio, akachukua uwezo wangu wa kuona na nikapoteza macho yangu ili nisishuhudie hali hii ya kutisha.

Wakati Hadhrat Abu Usaid alipokuja kwa ajili ya kugawa Zaka. Aliondoka baada ya kugawa kila kitu. Aliporudi nyumbani, alipitiwa na usingizi na akaona katika njozi nyoka amejivingirisha katika shingo yake. Aliamka kwa sababu ya kusumbuliwa na njozi hiyo na akamuuliza aidha mtumishi wake wa kike au mkewe kama kuna chochote alichokiacha kutoka katika mali aliyotakiwa kuitoa? Akasema hapana. Hadhrat Abu Usaid r.a akajibu kwa nini sasa nyoka alijiviringisha katika shingo yangu? Nenda ukaangalie. Huenda kuna kitu tumekiacha. Alipoenda kukagua, akasema kwa hakika, kuna kamba ya kufungia ngamia, ambayo pia ilikuwa inatumika kufungia ule mfuko(wa Michango). Kwa hiyo, Hadhrat Abu Usaid r.a akaenda kuirudisha kamba hiyo pia. Allah Alipenda Kuwawezesha Masahaba hawa wa Mtukufu Mtume s.a.w kukanyaga katika njia ngumu ya Ucha Mungu na kufikia viwango vya juu vya kurudisha Amana walioaminiwa kwayo. Hii ndio sababu walipewa muongozo hata katika njozi.

Ammarah bin Radhiya r.a anasimulia kauli hii ya Baba yake kuwa baadhi ya vijana walimuliza Hadhrat Abu Usaid r.a kuhusiana na ubora ambao MtukufuMtume s.a.w aliutaja juu ya Ansar(Waislam ambao ni wenyeji wa Madina). Kuhusiana na hili nilimsikia Mtume s.a.w akisema, kutoka miongoni mwa makabila ya Ansar, koo bora ni zile za Banu Najjar, kisha Banu' Abdul Ash'al, kisha Banu Harith bin Khazraj na kisha Banu Sa'da. Kisha akasema zaidi kuwa kila ukoo wa Ansar umejazwa na wema. Kuhusiana na hili, Hadhrat Abu Usaid alikuwa akisema kuwa ikiwa kama nitakiwe kukubali jambo lolote lakini liwe la imani, basi ningeanza na watu kutoka miongoni mwa Banu Sa'da.

Kwa kurejea tukio moja la kihistoria, Hadhrat Musleh Maud ra alisema katika sehemu moja kipindi Uarabuni ilipochukuliwa chini ya Waislamu na Uislamu ukaanza kusambaa, kulikuwa na Mwanamke moja kutoka katika kabila la Qinda, aliyejulikana kama Asma au Umaima, ambaye pia aliitwa kwa jina la Junia au Bint-ul- Jaun. Kaka yake Luqman alikuja kwa Mtukufu Mtume s.a.w akiwa kama muwakilishi wa kabila lao. Katika tukio hio alielezea mapenzi yake ya kutaka kuunga udugu kupitia ndoa ya Dada yake kwa Mtukufu Mtume s.a.w.

Kwa kuwa Mtume Mtukufu (saw) alitaka kuyaunganisha makabila ya Kiarabu, alimkubalia ombi lake hilo. Bibi huyo alijulikana kwa urembo wake na baadhi ya wanawake fulani walimuongoza vibaya. Baada ya Nika, Hadhrat Abu Usaid alimsindikiza mpaka Madina. Mtume Mtukufu (saw) alipokwenda kwenye nyumba iliyopangwa kwa ajili ya bibi huyo, bibi huyo akatoa maneno ya chuki sana yasiyo na mantiki akisema kwamba 'nina jikinga kwa Allah dhidi yako'. Aliposikia maneno ya bibi huyo Mtume Mtukufu (saw) mara moja akasema 'umeomba hifadhi na ulinzi toka kwa Aliye juu kabisa, Ambaye Anatoa ulinzi kwa wingi mno. Kwa hiyo, ninakukubalia ombi lako.' Hivyo, Mtume Mtukufu (saw) mara moja akatoka nje ya nyumba hiyo na akasema "Ee Abu Usaid! Mpe vipande viwili vya nguo na mrudishe kwao". Hivyo, kufuatia hilo, mbali na mahari yake, Mtume Mtukufu (saw) aliagiza apewe vipande viwili vya nguo ikiwa ni ishara ya wema. Sawa na amri ya Qur'an Tukufu (Al Baqara: 238) 'Msisahau kutendeana kwa wema' Mtume

Endelea uk. 11

Naipenda Jumuiya ya Islam Ahmadiyya - Paramaganda Kabudi

Na **Mwandishi Wetu**, Sabasaba DSM



Waziri wa Katiba na Sheria Mh. Paramaganda Kabudi akipokea zawadi ya Quran Tukufu katika banda letu la maonyesho Sabasaba mwaka 2017

Kwa mwaka wa pili mfululizo, Waziri wa Sheria na Katiba wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Paramaganda Kabudi amepata fursa ya kutembelea banda la Ahmadiyya katika viwanja vya sabasaba na kununua vitabu kadhaa vya kidini.

Naitambua Jumuiya hii, napenda kusoma vitabu vyenu na misimamo yenu naifahamu na naendelea kujifunza kupitia maandishi yenu lazima nikiri kuwa naipenda Jumuiya ya Ahmadiyya, alisema Mh. Kabudi alipotembelea tena wakati wa maonyesho hayo ya mwaka huu na kupata fursa ya kuonana na baadhi ya viongozi wa Jumuiya hii waliokuwepo bandani hapo na kumpokea.

Chanzo chetu cha kuaminika kimetueleza kuwa bwana Paramaganda Kabudi alikuwa mwandishi wa habari akilitumikia gazeti la Uhuru na Mzalendo.

Wakati akiwa Uhuru na Mzalendo ndipo alipokutana na Sheikh Saadani Abdul Kandoro, mmoja wa waasisi wa TANU na mshairi maarufu na Mhariri wa mashairi katika magazeti hayo mawili ya Uhuru na Mzaendo. Ambaye pia ndiye aliyemuhimiza Mh. Paramaganda Kabudi kusoma vitabu vya Ahmadiyya na kusoma mashairi ya Sheikh Kaluta Amri Abedi ambaye ni mpwaye. Ni jambo la kufurahisha kuwa Kabudi anakalia kiti alichotumia Sheikh Kaluta Amri Abedi alipokuwa Waziri wa Sheria 1963.

Maonyesho hayo yalihudhuriwa na maelfu ya watu wakiwemo raia wa kawaida, wafanyabiashara, wanasiasa na viongozi wa kidini ambao angalau waliwakilishwa na Jumuiya ya Waislam ya Ahmadiyya katika maonyesho hayo, yameacha athari kubwa kwa wale waliotembelea bandani hapo.



Waziri wa Katiba na Sheria Mh. Paramaganda Kabudi akipokea zawadi ya vitabu kutoka kwa Katibu wa Tahrik Jadid Taifa Amiri Kaluta sahib (kushoto) huku Sadr Khuddam Ramaddhani Nauja sahib (kulia) akishuhudia katika banda letu la maonyesho Sabasaba mwaka 2018